

HOTUBA YA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGORO NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA HAFLA YA UTIAJI SAINI MIKATABA 33 YA KAZI ZA BARABARA KATI YA TARURA NA WAKANDARASI KATIKA UKUMBI WA RDC TAREHE 12 AGOSTI,2024.

- *Ndugu Mwenyekiti wa CCM Mkoa,*
- *Kaimu Katibu Tawala Mkoa,*
- *Mjumbe wa Halmashauri kuu ya CCM Taifa (MNEC),*
- *Katibu wa CCM Mkoa,*
- *Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,*
- *Waheshimiwa Wabunge,*
- *Wakuu wa Seksheni na Vitengo wa Sekretarieti ya Mkoa,*
- *Katibu Tawala Msaidizi Miundombinu,*
- *Mstahiki Meya wa Manispaa ya Sumbawanga,*
- *Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya,*
- *Meneja TARURA Mkoa,*
- *Wakurugenzi wa Halmashauri,*
- *Mwenyekiti wa Wakandarasi,*
- *Wakandarasi,*
- *Viongozi wa Vyama vya Siasa,*
- *Machifu,*
- *Wazee Maarufu,*
- *Waandishi wa Habari,*
- *Wageni waalikwa,*
- *Mabibi na Mabwana.*

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....

Awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha sisi sote kukutana mahali hapa tukiwa wazima na wenye afya njema. Kipekee nikupongeze wewe Katibu Tawala Mkoa Pamoja na timu yako ya Seksheni ya Miundombinu na TARURA kwa kuona umuhimu wa kuandaa hafla hii ya kushuhudia utiaji saini wa mikataba 33 ya matengenezo ya Barabara za TARURA .

Ndugu Washiriki, Barabara zetu nyingi katika Msimu wa Mvua wa mwaka 2023/2024 ziliharibiwa na Mvua kubwa zilizo nyesha katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wetu. Ni faraja kubwa kwangu kuona hii leo Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametoa fedha kwaajili ya Matengenezo ya Barabara zetu na hatimae leo tunashuhudia utiaji Saini wa Mikataba 33 yenye thamani ya shilingi Bilioni **7,737,570,444.50**. Fedha hizi ni nyingi na zitaenda kuboresha kwa kiwango kikubwa Barabara zetu za Mijini na Vijijini katika Mkoa wetu wa Rukwa.

Ndugu Washiriki, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi **ibara ya 57** inasema kuwa “Kwa kutambua umuhimu wa kuendelea kuboresha miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi katika kuwezesha shughuli za kiuchumi na kijamii mijini na vijijini, Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka mitano 2020 - 2025 kitahakikisha Miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi inaboreshwa kwa lengo la kufungua fursa za kiuchumi na kijamii katika maeneo ya mijini na vijijini”. Kutokana na msisitizo huo wa Ilani ya Uchaguzi Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upendo mkubwa kwa Wanarukwa ambapo Bajeti ya

Barabara za TARURA kwa Mkoa wa Rukwa imeongezeka kutoka shilingi Bilioni 5.19 mwaka 2020/2021 hadi kufikia shilingi Bilioni **11.84 mwaka 2024/2025.**

Ndugu Washiriki, leo tunashuhudia utiaji saini wa Mikataba 33 kati ya TARURA na wakandarasi yenye jumla ya shilingi **Bilioni 7,737,570,444.50** kwaajili ya kutekeleza kazi mbalimbali za ujenzi na Matengenezo ya barabara, Madaraja na Makalvati, Mikataba hii ni ya awamu ya kwanza kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na awamu ya pili kazi zake bado zipo kwenye hatua ya manunuzi ambayo tunategemea itakamilika haraka iwezekanavyo. Nitoe rai yangu kwa TARURA kuhakikisha kuwa kazi zote zinakamilika katika muda uliopangwa na kwa mujibu wa BOQ na Mikataba. Aidha BOQ na Mikataba hiyo Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na TAKUKURU wapewe nakala ili kurahisisha ufuatiliaji. Hata hivyo niagize kwamba Ofisi yangu ipate nakala ya Mikataba hiyo na Mpango kazi wa utekelezaji wa Miradi yote.

Ndugu Washiriki, Kufanya Hafla ya kusaini Mikataba kunawasaidia Viongozi na Wananchi kujua Miradi inayokwenda kutekelezwa kwenye maeneo yao. Ni rai yangu kuwa Sekta zingine zitaiga mfano huu mzuri wa TARURA kwa kuhakikisha kuwa zinaandaa hafla za kusaini Mikataba ili Viongozi na Wananchi wajue Miradi inayoenda kutekelezwa kwenye maeneo yao ili kuweka uwazi na uwajibikaji kwa Wananchi.

Ndugu Washiriki, Kumekuwa na tabia kwa baadhi ya Wakandarasi wasio waaminifu kuomba kazi ambazo hawana uwezo nazo na mwishowe hutelekeza kazi hizo au kuzifanya chini ya kiwango. Kwa kuwa Wakandarasi wote mpo hapa niwaombe mfanye kazi zenu kwa uaminifu, uadilifu na uzalendo kulingana na mikataba yenu huku mkijua kuwa fedha hizo ni za Watanzania ambazo zimetolewa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili ziwanufaishe Wananchi. Hivyo kufanya kinyume na maelekezo ya mikataba ni kukiuka makubaliano na kuwaangusha Wanarukwa.

Mwisho, Nitoe shukrani zangu za dhati kwa Washiriki wa zoezi hili la utiaji saini wa Mikataba, ni Imani yangu kuwa Barabara hizo pamoja na makalavati na Madaraja zitajengwa kwa kiwango kilichokusudiwa na Mhe. Rais ili kuwarahisishia Wananchi wa Mkoa wa Rukwa ambao kwa asilimia kubwa ni Wakulima ili waweze kusafirisha mazao yao kwenda Sokoni.

Mungu Ibariki Tanzania!!!!!!

Mungu Bariki Mkoa wa Rukwa!!!!!!

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

Charles Makongoro Nyerere

MKUU WA MKOA RUKWA